
# Mwelekeo wa Msimu wa Mvua kwa Ngazi ya Mkoa na Wilaya zake

**MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2023 KWA MKOA WA KUSINI, PEMBA**
**Umetolewa: 24/08/2023**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba - Disemba, 2023; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali katika mkoa wa Kusini na wilaya zake:

(I) Ngazi ya Mkoa




Kielelezo 1: (a) Mwelekeo wa msimu wa Vuli, 2023 kwa kisiwa cha Pemba. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Vuli katika sehemu mbalimbali za kisiwa cha Pemba. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

**Dondoo**

(i) *Msimu huu unatarajiwa kutawaliwa na hali ya El Nino ambayo inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika mwenendo wa mvua za msimu wa Vuli, 2023.*
(ii) *Kwa ujumla mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mkoa wa Kusini, Pemba.*
(iii) *Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2023.*
(iv) *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Januari, 2024.*
(v) *Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli.*

**Mvua za msimu wa Vuli, 2023**
Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya wilaya za mkoa wa Kusini, Pemba.

***Angalizo:***
*Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani.*

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Chuo kikuu cha Dodoma, Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz


**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727N – 00/2023*

(II) Ngazi ya Wilaya

**MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2023 KWA WILAYA YA CHAKE CHAKE**
**Umetolewa: 24/08/2023**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2023; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Chake Chake.




Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2023 kwa wilaya ya Chake Chake, Pemba

### Dondoo muhimu

*(i). Mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Chake Chake.*
*(ii). Mvua zitaanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2023.*
*(iii). Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya kwanza na ya pili mwezi Januari, 2024.*
*(iv). Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.*

## Mvua za msimu wa Vuli, 2023 kwa wilaya ya Chake Chake

**Zitaanza:** Wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2023.

**Zitaisha:** Wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Januari, 2024.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa juu ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Chake Chake ni kati ya milimita 320 hadi 380.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2023.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2023.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa nyingi na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

## Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

### Matokeo

(i). Wadudu waharibifu na mlipuko wa magonjwa ya mifugo na mazao yanayoambatana na mvua nyingi yanaweza kujitokeza.
(ii). Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri mazao pamoja na miundombinu ya kilimo.
(iii). Upatikanaji wa chakula cha Samaki na malisho ya mifugo unatarajiwa kuongezeka.

### Ushauri

(i). Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.
(ii). Matumizi sahihi ya mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji shambani, mmomonyoko na upotevu wa rutuba, vinashauriwa.
(iii). Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae.
(iv). Wavuvi na wafugaji wa samaki wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya uvuvi na ufugaji wa samaki.




*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Chuo kikuu cha Dodoma, Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz




**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

727N – 00/2023

(II) Ngazi ya Wilaya

**MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2023 KWA WILAYA YA MKOANI**
**Umetolewa: 24/08/2023**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2023; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Mkoani.




Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2023 kwa wilaya ya Mkoani, Pemba

### Dondoo muhimu

*(i). Mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Mkoani.*

*(ii). Mvua zitaanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2023.*

*(iii). Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya kwanza na ya pili mwezi Januari, 2024.*

*(iv). Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.*

## Mvua za msimu wa Vuli, 2023 kwa wilaya ya Mkoani

**Zitaanza:** Wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2023.

**Zitaisha:** Wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Januari, 2024.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa juu ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Mkoani ni kati ya milimita 320 hadi 380.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2023.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2023.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa nyingi na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

## Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

### Matokeo

(iv). Wadudu waharibifu na mlipuko wa magonjwa ya mifugo na mazao yanayoambatana na mvua nyingi yanaweza kujitokeza.

(v). Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri mazao pamoja na miundombinu ya kilimo.

(vi). Upatikanaji wa chakula cha Samaki na malisho ya mifugo unatarajiwa kuongezeka.

### Ushauri

(v). Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.

(vi). Matumizi sahihi ya mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji shambani, mmomonyoko na upotevu wa rutuba, vinashauriwa.

(vii). Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae.

(viii). Wavuvi na wafugaji wa samaki wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya uvuvi na ufugaji wa samaki.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Chuo kikuu cha Dodoma, Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz



**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**